KANISA LA AFRIKA
LAPAMBANA NA JANGA LA UKIMWI:
"Nyakati zote maombi yetu yamejaa matumaini"

UJUMBE ULIOTOLEWA NA SECAM (SHIRIKISHO LA MAASKOFU WA AFRIKA NA MADAGASCAR)
DAKAR 2003

Wapendwa katika imani,
Marafiki, waumini wenzetu na watu wote wenye mapenzi mema,

"Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo" (1Kor 1:3).

Sisi Makardinali, Maaskofu wakuu na Maaskofu wote wa Afrika na Madagascar, twawasalimu ninyi wote katika imani na kwa upendo. Tulipokutana katika Mkutano wetu Mkuu wa 13 wa Maaskofu wa Afrika na Madagascar" (SECAM), tulijadili mada ya UKIMWI na athari zake mbaya kijamii. Kwa kufanya hivyo, tumeungana nanyi ndugu zetu waathirika, na wale wote waliochukua jukumu la kupigana na janga la UKIMWI na athari zake.

I TUMESHIKAMANA/ TUMEUNGANA

"Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja, vivyo hivyo na Kristo". (1Kor 12:12)

Picha hii bora inafafanua vyema mshikamano tunaopaswa kuuonyesha kwa wale wote wanaoathirika, lakini zaidi kwa kaka na dada zetu katika Kristo, ambao ni **mwili mmoja, pamoja na mamilioni ya wengineo wanaounda jumuiya ya Wakristu ya Afrika na Madagascar. Ni kwenu ninyi ndipo tunapouelekeza wito wetu ili tushikamane kulikabili janga hili ambalo madhara yake hayawezi kuchukuliwa kimzaha na yeyote yule.**

Vyema mshikamano huu uambatanishwe na ufahamu wa madhara ya kuogofya ya janga hili linalotusibu. Mamilioni ya maisha yamepotea yakingali machanga, familia zimeteketea au kusambaratika, na idadi isiyohesabika ya watoto sasa ni yatima na/au ni waathirika. Na hawa, kuliko wote, ndio wanaohitaji matunzo, malezi, makao, elimu na watu wazima wa kuwalea.

II TUWE WAAMINIFU KWA NAFSI ZETU

Sisi kama viongozi wa Jumuiya zetu za Kikristo, **tunajitoa ili kuhakikisha kuwa raslimali ya Kanisa**, iwe vyombo vya elimu, afya na huduma za kijamaa, vinakuwepo ili kuuhudumia umma. Tutashirikiana na wafadhili wote ambao wako radhi kusaidia na kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi za Kikristu na za Kidini. Tuko radhi kushirikiana nao wote na **wale wote walio tayari kutumia vipawa vyao katika mapambano haya, huku wakifanya hivyo kwa kufahamu kuwa sisi tunatenda hivyo kufuatia imani yetu katika Injili**. Maana, "*mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu*" (Mt. 4:4).

Maadili tuyafundishayo katika jina la Mungu yanalenga kuheshimu na kuhakiki umuhimu wa uhai wa binadamu, ambao unatunukiwa, kupata thamani na ubora wake kufuatia ukweli thabiti ya kuwa "uhai ni zawadi isiyoweza kudhulumiwa au kudhalilishwa itokayo kwa Mungu Baba anayemwumba kila binadamu na kuwaita wote kwenye utimilifu wa kimaisha". Hivyo basi, kujinyima vitendo vya ngono na uaminifu siyo tu njia bora za kuepukana na maambukizi ya UKIMWI au kuwaambukiza wengine, bali pia ni njia bora zihakikishazo mwendelezo wa furaha ya kudumu ya kimaisha na namna ya kufikia utimilifu kamili wa kimaisha.

"*Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana*" (1 Kor 15:58).

III TUBADILI MIENENDO

Licha ya kufundisha maadili ya Kikanisa na kuchangia ueleo wetu wa maadili na jamii nzima, na licha ya kuwaelewesha na kuwatahadharisha watu juu ya athari za maambukizi ya UKIMWI, **tunataka kuielimisha jamii kiusahihi na kuboresha maadili ya kubadili tabia na mienendo** tukuzingatia uzuri wa kujinyima vitendo vya ngono, kujidhibiti kabla ya ndoa na uaminifu katika ndoa. Tunalenga kuuelimisha umma juu ya "upendo halisi" na elimu ya kijinsia, ili kuwasaidia vijana na wanandoa wazidi kuvumbua uzuri na ubora wa jinsia zao na baraka ya uwezo wao wa kuzaa. Kutokana na uzuri na ubora huo uhusiano wa kujamiiana unapata heshima na kutumiwa kwa namna inayowawajibisha wahusika, na pia udhibiti wa mpango wa uzazi kati ya mke na mume unakuwa wa kuheshimiana.

Elimu hii yaweza kuboreshwa na kufanikiwa kama ushirikiano hai wa walei, wake kwa waume, wote ambao wamekuwa si tu wakiongelea juu ya taratibu za kimaadili, bali pia katika ujana wao na kama wanaondoa, wanatoa ushuhuda hai ya kuwa taratibu na maadili mema huzaa mahusiano ya kujamiiana yanayoleta uhusiano bora na upendo wa kibinadamu, na uwajibikaji katika ngono. **Elimu hii pia huchangia katika kuunda familia bora na imara, ambazo kwazo tunapata kinga bora dhidi ya ukimwi**. Asasi[1] zilizobobea katika utoaji wa elimu ya namna hii kwa vijana na wanandoa zimetapakaa pote Afrika na zimekuwa zikizaa matunda ya kutia moyo, licha ya kuwa yaonekana kuwa kidogo. Zote hizi tunazitia moyo na mhimizo unaozistahili.

IV TUWAJIBIKE

Mshikamano tuliouongelea hapo awali unatuunganisha na kutuwajibisha sote katika kukabiliana na changamoto ngumu zenye sura ya utandawazi: vita sugu na zisizo na vikomo, migogoro na fujo zinazohusisha ubakaji mara nyingine kama silaha – hii siyo tu kama ni udhalilisho wa kisaikolojia bali pia ni uangamizaji jamii kwa jinsi unavyoambukiza na kusambaza UKIMWI.

Tumegundua pia kwamba **umaskini huenda sambamba na UKIMWI.** Inatukereketa sana kuona kuwa uchumi wetu legelege unazidi kudidimia kufuatia

[1] Education for Life, Youth Alive, *Action Familiale, Pro Vita* (Tafsiri yetu wenyewe).

vifo vya wafanyakazi wataalamu na wanataaluma kutokana na gonjwa la UKIMWI. Umaskini unachangia usambazaji wa virusi vya UKIMWI, unafanya matibabu na dawa za kinga yawe aghali, unasaidia kuharakisha vifo kwa waathirika na unazidisha athari za gonjwa hili kijamii.

Katika haya yote, *"Basi kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane, kila kiungo na mwenziwe" (1 Kor 12:25).* **Mshikamano** huu kati yetu na **uaminifu** wa imani yetu, uamuzi thabiti wa kubadili **mienendo** na **kuwajibika** kwetu kwa ajili ya umbele wa bara letu, vyote sasa vinapata sura kamili na uelekeo kufuatia Mikakati ya Kiuetendaji ifuatayo. Tunaiweka mikakati hii mbele yenu muitumie kwa manufaa yenu.

Mikakati ya Kiutendaji

Sisi Makardinali, Maaskofu wakuu na Maaskofu wa Afrika na Madagascar, SECAM, tunapendekeza kwa wakleri, mabruda, watawa wa kike na kiume, waumini na watu wote wenye mapenzi mema, mikakati ifuatayo ya kiutendaji.[2]

I. **Tukishikamana nanyi, tunaazimia:**

1. Kutumia vyema na kuimarisha vigezo na vipawa vya kibinadamu, vya hali na mali/fedha - ambavyo tayari vimetengwa ili kukabiliana na janga la UKIMWI katika jumuiya zetu, na kuainisha vipengele vya muhimu kiparokia, jimbo na Baraza la Maaskofu mahalia ili kusaidia kukusanya takwimu na taarifa muafaka, na mipango ya kimaendeleo. Katika hili pia tunaazamia kuunganisha uratibu wa jitihada zetu kwenye ngazi ya bara zima ili kupambana na janga la UKIMWI.

2. Kuhakikisha ya kuwa huduma za kiafya za Kanisa, huduma za Kijamii na taasisi za elimu zinawajibika ipasavyo kukidhi mahitaji ya waathirika wote.

3. Kuwalenga wanyonge katika jamii, hasa wasichana na kinamama wanaobeba mzigo mkubwa kijamii tunapoiangalia hali halisi na athari za janga la UKIMWI hapa Afrika.

4. Kuhamasisha kwa bidii upatikanaji wa matibabu kwa wote wasioweza au wanazuiliwa kupata matibabu hayo kufuatia umaskini wao na uonevu wa kijamii.

[2] Msingi wa mapendekezo haya ni "Mikakati ya Utekelezaji" kadri ilivyotayarishwa na Mkutano wa Viongozi wa Kidini kuhusu Mtoto na UKIMWI, Nairobi 9 – 12 Juni 2002, na Mapendekezo ya Mikakati ya Kiutekelezaji kuhusu UKIMWI yaliyoandaliwa na Makatibu Wakuu wa SECAM, Johannesbung 24 – 27 Oktoba 2002

5. Kuwahusisha kiutafiti wale wote walio waliobobea katika dawa asilia/ za kienyeji na kinga asilia ili kufikia ufumbuzi na upatikanaji wa njia bora za kujikinga na kupambana na janga la UKIMWI.

II. Huku tukiwa waaminifu kwa tunu zetu za Kiinjili, tunaazimia:

1. Kushirikiana na Wakristu wa madhehebu mengine na dini nyinginezo ambao wanafanya kazi katika jumuiya zao ili kuwasaidia waathirika.

2. Kuhamasisha uhusiano wa karibu zaidi na jamii, sekta binafsi/wafanyabiashara, serikali, Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Kimataifa, na taasisi za kiserikali na hasa asasi za kuwahudumia waathirika, ili kuinua na kuboresha uwezo wake katika kuwatunza na kuwahudumia waathirika, bila kupotosha tunu zetu za kiinjili.

III. Tukikabiliana na tishio la UKIMWI, tunaazimia pamoja nanyi:

1. Kuhamasisha mabadiliko ya kitabia, mienendo na maadili husika katika kupambana na changamoto la UKIMWI.

2. Kujibidiisha bila kuchoka ili kuondoa dhana potofu dhidi ya waathirika na kuwatenga/kuwabagua kijamii, na kuzipa changamoto taratibu za kijamii, kidini, kitamaduni na kisiasa na mapokeo yote yanayoendeleza hisia potofu zisababishazo kutengwa/kubaguliwa kijamii kwa waathirika.

3. Kuwa msitari wa mbele katika kufutilia mbali dhana potofu dhidi ya waathirika na ubaguzi wa kijamii kwa kuhamasisha Ushauri na Upimaji Huru (Voluntary Councelling and Testing, VCT), ili waathirika waweze kufaidika na matunzo na huduma wanazozihitaji. Hii itasaidia pia kuthibiti uambukizaji kati ya mama na mtoto.

4. Kuhamasisha bega kwa bega pamoja na ngazi zote za serikali, na asasi zake juu ya utunzi wa miongozo ipasayo kupewa kipaumbele na ambayo itasaidia vyema kuwahudumia waathirika, kuwaruhusu waathirika kupata huduma na matibabu, kutunza na kuuheshimu utu wao katika jamii, na kuyatendea kazi maazimio yote yaliyofikiwa katika vikao vya asasi za kiserikali.

IV Tukiwajibika kwa pamoja, tunaazimia:

1. Kubuni na kuendeleza mikakati ya kielimu inayoshirikisha mada za UKIMWI hasa katika nyanja za tauhidi na malezi ya kitawa.

2. Kuhamasisha na kuimarisha kwa undani zaidi tafakari za kitauhidi kuhusiana na tunu za huruma, upendo, uponyaji, upatanishi na matumaini, ambazo kwa pamoja zinaweza kupambana na vizingiti vya hukumu, aibu na woga - ambavyo mara nyingi huambatana na athari za UKIMWI (vikiwalenga waathirika).

3. Kuandaa warsha kwenye ngazi za kikanda, kitaifa, kijimbo na kiparokia ili kuboresha na kukuza upeo, kuleta ufahamu na maarifa kuhusu UKIMWI; na kuleta mwamko kuhusiana na masuala ya UKIMWI – kuwaelewesha vyema wahusika wote msimamo na maadili ya Kanisa kuhusu janga hili.

V. Mwisho, sisi kama <u>wachungaji wa Kanisa - Familia ya Mungu hapa Afrika kwenye kipindi kigumu cha UKIMWI</u>, tunaazimia:

1. Kuwaanda vvyema kitaaluma wakleri, watawa na walei walio na moyo wa kujituma ili waambatane na waathirika katika sala na mashauri ya kiroho.

2. Kutoa malezi kuhusiana na mafundisho ya Kanisa, malezi ya kiroho na kijamii – na mafunzo bora katika taaluma za elimu dunia, kwa wale wote walio na wito wa kuwahudumia na kuambatana na waathirika.

3. Kuwapokea waathirika makanisani kwa moyo wa upendo na huruma, bila kuwahukumu, na "kuwahakikishia nafazi zao mezani mwa Bwana."

4. Kuwapatia sakramenti na huduma za kikanisa kwa taratibu zilizo sahihi na kadri ilivyoombwa na Wakatoliki waathirika.

5. Kulitendea kazi changamoto lililotolewa na Baba Mtakatifu Yohani Paulo II kwa makanisa ya bara letu kupitia Wito wake wa Kitume, *Apostolic Exhortation*, Kanisa Barani Afrika, *Ecclesia in Africa*:

   "Vita dhidi ya UKIMWI ni ya kila mmoja wetu. Nikirudia wito wa Mababa wa Sinodi, nami natoa wito kwa wahudumu wa kichungaji kuleta kwa waathirika, makaka na madada, kadri iwezekanavyo tulizo la mahitaji ya kimwili, morali na kiroho. Huku nikihimiza, nawaomba viongozi wa nyanja za kisayansi na kisiasa, wakisukumwa na pendo na heshima inayomstahili kila binadamu, watumie kwa busara njia zote ziwezekanazo ili kusitisha athari za janga hili".[3]

Tunadhamiria kuunda kitengo cha huduma kuhusu UKIMWI kwenye ngazi ya bara zima la Afrika ili kitusaidie kutekeleza Mikakati yetu ya Kiutekelezaji.

(Imetiwa sahihi) Kongomano la Shirikisho la Mabaraza ya Kiaskofu - Afrika na Madagascar (SECAM) Dakar, Senegal, 7/10/2003.

Fr. Peter Lwaminda
SECAM General Secretary
P.O.Box KA 9156, Airport
Accra, GHANA

e-mail: secamsecr@internetghana.com

fax: (+233.21) 778 867 or 778 678

[3] Pope John Paul II, *Ecclesia in Africa*, 14 September 1995, #116.